

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*Supplement No. 44*

*22<sup>nd</sup> November, 2022*

***SPECIAL SUPPLEMENT***

*To The Special Gazette Of The United Republic Of Tanzania No. 44 Vol. 103 Dated 22<sup>nd</sup> November, 2022  
Printed By The Government Printer, Dodoma By Order Of Government*

---

TANGAZO LA SERIKALI Na. 658A La Tarehe. 22/11/2022

SHERIA YA USIMAMIZI WA MAAFA,  
(NA. 6 YA MWAKA 2022)

—————  
**KANUNI**  
—————

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 40)*  
—————

KANUNI ZA USIMAMIZI WA MAAFA ZA MWAKA 2022

SEHEMU YA KWANZA

MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI  
KITUO CHA OPERESHENI NA  
MAWASILIANO YA DHARURA

3. Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura.
4. Kazi za Kituo.
5. Uamshaji wa Kituo.
6. Uanzishwaji wa vituo vya operesheni na mawasiliano ya dharura vya kisekta na ngazi ya mkoa na wilaya.

SEHEMU YA TATU  
USIMAMIZI NA URATIBU WA MAAFA

7. Utaratibu wa utekelezaji wa mamlaka ya Waziri.
8. Makazi ya waathirika.
9. Utoaji taarifa za usimamizi wa maafa.
10. Uwasilishaji wa taarifa.
11. Utaratibu wa matumizi ya fedha za Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa.
12. Majukumu ya Serikali za Mitaa.
13. Majukumu ya taasisi za Serikali.
14. Mpango wa Usimamizi wa Maafa na Mpango wa Mwendelezo wa Huduma wakati wa Dharura ya Kitaifa.
15. Ngazi za kushughulikia maafa.
16. Tathmini ya eneo la maafa.
17. Timu ya tathmini ya madhara na mahitaji.
18. Notisi ya kuondoka.
19. Notisi ya kurudi katika makazi ya awali au kwenda katika eneo salama.
20. Notisi ya kubaki katika sehemu ambapo mtu yupo.
21. Notisi ya kuendelea na shughuli za kijamii na kiuchumi.

- SEHEMU YA NNE  
UTARATIBU WA KUJITOLEA KATIKA USIMAMIZI WA MAAFA
22. Ushiriki wa wanaojitolea katika usimamizi wa maafa.
  23. Majibu ya ombi la kujitolea na ukomo wa kujitolea.
  24. Kuanzishwa na ushiriki wa klabu katika shughuli za usimamizi wa maafa.

SEHEMU YA TANO  
MASHARTI YA JUMLA

25. Utoaji wa taarifa.
26. Masharti kuhusu ukusanyaji wa misaada na michango wakati wa maafa.
27. Ghala la kuhifadhia misaada ya kibinadamu.
28. Rejesta ya kutoa na kupokea misaada ya kibinadamu.
29. Makosa na adhabu.
30. Kufutwa kwa Kanuni za Usimamizi wa Maafa za Mwaka 2017.

SHERIA YA USIMAMIZI WA MAAFA,  
(NA. 6 YA MWAKA 2022)

**KANUNI**

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 40)*

KANUNI ZA USIMAMIZI WA MAAFA ZA MWAKA 2022

SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZI

- Jina. 1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Usimamizi wa Maafa za Mwaka 2022.
- Tafsiri 2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-  
“Divisheni” ina maana sawa na maana iliyotolewa kwenye Sheria.  
“jeshi” maana yake ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi Tanzania, Jeshi la Uhamiaji, Jeshi la Magereza na Jeshi la Zima Moto na Uokoaji;  
“Katibu Mkuu” ina maana sawa na maana iliyotolewa kwenye Sheria;  
“Kituo” maana yake ni sawa kama ilivyotolewa kwenye Sheria;  
“makundi maalum” inajumuisha watoto, wajawazito, wazee, watu wenye ulemavu, watu wenye utapiamlo, wakimbizi, wahamiaji wa ndani, watu wenye magonjwa ya muda mrefu na upungufu wa kinga;  
“Sheria” maana yake ni Sheria ya Usimamizi wa Maafa;  
“usaidizi wa kijeshi kwa mamlaka za kiraia” maana yake ni usaidizi unaotolewa kwa mamlaka za kiraia na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika usimamizi wa maafa; na  
“Waziri” inamaana sawa na maana iliyotolewa kwenye Sheria.
- Na. 6 ya mwaka 2022

SEHEMU YA PILI  
KITUO CHA OPARESHENI NA MAWASILIANO YA DHARURA

Kituo cha  
Oparesheni na  
Mawasiliano  
ya Dharura

3.-(1) Kituo kilichoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria, kitafanya kazi masaa ishirini na nne wakati wa dharura na kwa muda wa kawaida wa saa za kazi wa Serikali pasipokuwa na dharura chini ya usimamizi wa Divisheni.

(2) Katika kila chumba cha oparesheni cha Kituo, kutakuwa na vifaa na mifumo mbalimbali ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa kadri vitakavyohitajika, na vitajumuisha-

- (a) ramani ambazo zitawezesha eneo la maafa kuonekana vizuri ikijumuisha topografia au sura ya eneo husika, miundombinu muhimu ikiwemo barabara, reli, maji, nishati, mawasiliano, majengo ya umma, makazi, shughuli za kiuchumi ikiwemo kilimo, uvuvi na ufugaji, viwanda na maliasili zilizobainishwa ipasavyo;
- (b) taarifa ya mwenendo wa hali mbaya ya hewa, milipuko ya magonjwa kwa binadamu na wanyama, wadudu waharibifu wa mazao na majanga mengine kadri yatakavyojitokeza;
- (c) ubao unaoonesha takwimu za maafa, orodha ya wadau, vifaa vya utafutaji na uokoaji na vifaa vya misaada ya huduma ya kibinadamu;
- (d) luninga inayoonyesha picha za satelaiti ya hali ya eneo la maafa;
- (e) mifumo ya kiteknolojia ya habari ya mawasiliano na ya kijiografia kwa ajili ya ufuatiliaji wa mwenendo wa majanga, uchambuzi wa hali hatarishi na utoaji wa tahadhari ya mapema; na
- (f) wasifu wa maeneo mbalimbali unaoonesha aina ya majanga yanayoweza kutokea katika maeneo hayo.

Kazi za Kituo

4. Kazi za Kituo zitakuwa-

- (a) kupokea, kuchambua na kusambaza taarifa za

- maafa ndani na nje ya Nchi na taarifa kutoka katika vituo vya kisekta;
- (b) kuandaa taarifa za tahadhari ya mapema zinazohusu maafa ya kitaifa;
  - (c) kuratibu na kudhibiti oparesheni za maafa kitaifa;
  - (d) kuandaa itifaki kwa ajili ya usimamizi wa Kituo wakati wa hali ya dharura na hali ya dharura inayotazamiwa;
  - (e) kuratibu na kuanzisha vituo vidogo vya oparesheni kwenye maeneo yaliokumbwa na maafa;
  - (f) kufuatilia mwenendo wa janga na kukadiria eneo litakapotokea pamoja na kiwango cha madhara kwa maisha, miundombinu na mazingira na kushauri ipasavyo;
  - (g) kuandaa mfumo wa jukwaa la teknolojia ya mtandao wa tovuti ya mawasiliano wenye kutumia taarifa za jiografia kwa ajili ya kutoa tahadhari ya mapema kwa wakati na eneo husika;
  - (h) kuratibu na kusambaza taarifa zinazohusu masuala ya maafa;
  - (i) kushirikiana na vituo vya kisekta katika ngazi ya taifa, mikoa na wilaya ili kuhakikisha vinakuwa na mifumo ya kutoa na kupokea taarifa za majanga mbalimbali inayoendana na mahitaji ya Kituo cha Taifa; na
  - (j) kushirikiana na vituo vya kikanda na kimataifa kwa dharura zinazovuka mipaka.

Uamshaji wa Kituo

5.-(1) Kituo kitafanya kazi kwa kuzingatia taratibu za kuamsha na kuzima kama inavyohitajika ili kuchukua hatua za haraka wakati wa dharura .

(2) Uamshaji wa Kituo kwa sehemu au kamili utazingatia Mpango wa Kujiandaa na Kukabiliana na Dharura kwa kufuata mfumo wa ngazi tatu za uamshaji kituo kama ifuatavyo-

- (a) endapo tukio la dharura litasimamiwa na ngazi ya mkoa au wilaya, idara moja au zaidi pamoja

- na taasisi za serikali katika eneo husika, sehemu ya Kituo itaamshwa kufuatilia hali ya tukio;
- (b) endapo dharura itahitaji nguvu kubwa na rasilimali za ziada kutoka serikali kuu, idara na taasisi mbalimbali, Kituo kitaamshwa sehemu au chote ili kiweze kuratibu hali ya kukabili janga na maafa yaliyotokea;
- (c) endapo dharura itahitaji uratibu mkubwa na rasilimali nyingi kutoka idara na taasisi za serikali na kuhitaji msaada wa nchi nyingine au mashirika ya kutoa misaada ya kibinadamu ya kimataifa, Kituo chote kitaamshwa ili kiweze kuratibu hatua za kukabiliana na hali.

Uanzishwaji wa vituo vya kisekta katika ngazi ya Taifa, na vituo vya mkoa na Wilaya vya majanga mbalimbali.

6.-(1) Uanzishwaji wa vituo vya kisekta katika ngazi ya taifa, mkoa na wilaya utafanyika chini ya usimamizi wa ngazi husika kwa kushirikiana na Kituo.

(2) Kituo katika ngazi ya mkoa na wilaya kitakachoanzishwa kitahusika na ufuatiliaji wa matukio ya majanga ya aina zote.

(3) Vituo vya kisekta vitakavyoanzishwa katika ngazi ya taifa, mkoa na wilaya vitafanya kazi masaa ishirini na nne wakati wa dharura, endapo hakuna dharura muda wa vituo kufanya kazi utakuwa kwa kadri itakavyoamuliwa na sekta husika.

(4) Vituo vya kisekta vitakuwa na jukumu la kupokea taarifa za tahadhari za mapema zilizotolewa na Kituo na kusambaza katika ngazi husika kwa wananchi.

(5) Vituo vya kisekta vitakuwa na jukumu la kuandaa takwimu za matukio ya majanga, madhara yaliyotokea, shughuli zilizofanyika kukabili maafa pamoja na misaada iliyotolewa kwa waathirika na kuwasilisha taarifa kwa Katibu Mkuu kupitia kamati katika ngazi husika.

(6) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) taasisi, idara au mamlaka iliyoanzisha kituo cha dharura inawajibika kuwasilisha maombi ya kuunganisha kituo hicho na Kituo kwa Katibu Mkuu ikieleza mahali kituo kilipo, jukumu linalotekelezwa na uwezo wa kituo.

SEHEMU YA TATU  
USIMAMIZI NA URATIBU WA MAAFA

Utaratibu wa  
utekelezaji wa  
mamlaka ya  
Waziri

7.-(1) Katika kutekeleza mamlaka yake kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria, Waziri atazingatia utaratibu ufuatao:

- (a) kutoa tangazo kwa umma katika namna iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi-
  - (i) la kuwataka wananchi kuondoka kwenye eneo la maafa au hatarishi au kuwazuia wananchi kuondoka eneo husika ili kuwalinda dhidi ya maafa kupitia Gazeti la Serikali na vyombo vya habari vinavyopatikana katika eneo husika au kupitia njia nyingine zozote zinazofahamika katika eneo husika;
  - (ii) kusimamisha au kuzuia uzaji wa vileo, vinywaji, silaha, milipuko, au vitu vingine ambavyo vitaonekana havipaswi kuwa kwenye maeneo ya maafa;
- (b) kabla ya kuamuru matumizi ya rasilimali za idara, taasisi au mamlaka za serikali wakati wa shughuli za dharura, Waziri atazingatia yafuatayo:
  - (i) rasilimali hiyo iwe imeainishwa na Kamati Elekezi ya Kitaifa ya usimamizi wa maafa kuwa itumike.
  - (ii) ataijulisha idara, taasisi au mamlaka husika kuhusu nia ya Serikali kutumia rasilimali husika;
- (c) endapo rasilimali ya taasisi, idara au mamlaka iliyochukuliwa kwa amri ya Waziri na kutumika wakati wa shughuli za dharura ipo katika hali nzuri, inaweza kurejeshwa kwa idara, taasisi au mamlaka husika mara baada ya shughuli za kukabili maafa kukamilika;
- (d) maelekezo ya Waziri kwa idara, taasisi au mamlaka kuhusu shughuli za usimamizi wa

maafa yatajumuisha shughuli inayopaswa kutekelezwa, namna ya kuitekeleza, muda na mahali pa utekelezaji.

- (e) endapo maelekezo yaliyotolewa kwa mujibu wa aya (d) ya kanuni hii hayakutekelezwa ndani ya muda uliobainishwa bila sababu za msingi, Wizara itatekeleza kazi hizo au Waziri anaweza kuelekeza kazi hizo zitekelezwe na taasisi, idara au mamlaka nyingine kadri itakavyoonekana inafaa;
- (f) taasisi, idara au mamlaka iliyotekeleza shughuli kwa maelekezo ya Waziri kwa mujibu wa aya (e), itapaswa kubainisha gharama zilizotumika na kuziwasilisha kwa Waziri;
- (g) kwa kuzingatia aya (h) ya kanuni hii, mara baada ya Waziri kupokea gharama zilizotumika kutoka kwa taasisi, idara au mamlaka, ataziwasilisha kwa taasisi, idara au mamlaka ambayo ilipaswa kutekeleza jukumu hilo, na gharama husika zitakuwa ni deni kwa taasisi, idara au mamlaka hiyo.

Makazi ya waathirika

8.-(1) Divisheni itaandaa na kutunza orodha ya makazi au vituo vinavyoweza kutumika kama makazi baada ya taarifa ya tahadhari kutolewa au baada ya janga kutokea.

(2) Orodha ya makazi ya waathirika itajumuisha yafuatayo-

- (a) aina ya makazi;
- (b) vifaa na miundombinu katika kila makazi;
- (c) ubora wa kila makazi yanayopaswa kutumika baada ya taarifa ya tahadhari kutolewa au baada ya janga kutokea; na
- (d) muda na masharti ya matumizi ya makazi katika mazingira yaliyobainishwa katika aya (c).

Utoaji taarifa za usimamizi wa maafa

9.-(1) Taarifa za kila robo mwaka za usimamizi wa maafa au taarifa nyingine za usimamizi wa maafa za kamati za wataalam za mkoa za usimamizi wa maafa,



kamati za wataalam za jiji, manispaa, miji na wilaya za usimamizi wa maafa, kamati za kata za usimamizi wa maafa na kamati za vijiji au mitaa za usimamizi wa maafa zitajumuisha yafuatayo-

- (a) mipango na programu za usimamizi wa maafa zinazotekelezwa;
- (b) hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza matakwa ya mipango iliyoandaliwa kwa mujibu wa ya (a); na
- (c) oparesheni za dharura na misaada yote iliyoombwa na kutolewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maafa katika eneo husika.

(2) Taarifa kuhusu oparesheni za dharura itakayoandaliwa kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1) (c) itakuwa kama ilivyoinishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

Uwasilishaji  
wa taarifa

10.-(1) Taarifa zilizoandaliwa kwa mujibu wa kanuni ya 9 -

- (a) ikiwa ni taarifa ya kamati za vijiji au mitaa za usimamizi wa maafa, zitawasilishwa kwa kamati za kata za usimamizi wa maafa ndani ya siku saba baada ya robo mwaka kuisha;
- (b) ikiwa ni taarifa ya kamati za kata za usimamizi wa maafa, zitawasilishwa kwa kamati za wataalam za jiji, manispaa, miji na wilaya za usimamizi wa maafa ndani ya siku saba baada ya robo mwaka kuisha;
- (c) ikiwa ni taarifa ya kamati za wataalam za jiji, manispaa, miji na wilaya za usimamizi wa maafa, zitawasilishwa kwa kamati za wataalam za mikoa za usimamizi wa maafa ndani ya siku saba baada ya robo mwaka kuisha;
- (d) ikiwa ni taarifa ya Kamati za Wataalam za Mikoa za Usimamizi wa Maafa, zitawasilishwa kwa Kamati ya Wataalam ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa ndani ya siku saba tangu robo mwaka kuisha.

Utaratibu wa  
matumizi ya  
fedha za  
Mfuko wa  
Taifa wa  
Usimamizi wa  
Maafa

11.-(1) Fedha za Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa ulioanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha Sheria, zitatumika kwa shughuli za usimamizi wa maafa pekee kwa kuzingatia utaratibu ufuatao-

- (a) katika kuzuia na kupunguza madhara ya majanga, yafuatayo yatazingatiwa:
- (i) kutoa elimu kwa umma kuhusu njia za kuzuia na kupunguza madhara;
  - (ii) kuunda na kujenga uwezo kwa timu za dharura za utayari wa kujiandaa na kukabiliana na majanga;
  - (iii) kufanya tathmini ya vihatarishi vya majanga katika jamii;
  - (iv) kuandaa mipango ya dharura ya kuzuia, kupunguza madhara, kujiandaa na kukabili majanga;
  - (v) kuandaa mifumo jumuishi ya kupeana taarifa za tahadhari za mapema;
  - (vi) kuwezesha ujenzi wa miundombinu itakayosaidia kuzuia au kupunguza madhara ya majanga;
  - (vii) kuwezesha upatikanaji wa bidhaa au huduma zitakazosaidia kuimarisha mfumo wa maisha ya jamii ambayo iko katika hatari ya kuathirika na majanga;
  - (viii) shughuli nyingine za usimamizi wa maafa zinazohusiana na kuratibu, kuzuia na kupunguza madhara ya majanga;
- (b) katika kujiandaa kwa ajili ya maafa yanayoweza kutokea yafuatayo yatazingatiwa:
- (i) kujenga uwezo wa vifaa, utalam na mazoezi kwa kamati za usimamizi wa maafa na timu za kukabiliana na maafa;
  - (ii) kuimarisha mfumo wa mawasiliano na utoaji wa tahadhari ya mapema;
  - (iii) kuandaa mipango na miongozo ya kujiandaa na kukabiliana na maafa;
  - (iv) kutoa taarifa ya tahadhari ya mapema;

- (v) kutoa elimu kwa umma kuhusu njia za kujiandaa kwa ajili ya maafa yanayoweza kutokea;
  - (vi) utafutaji wa rasilimali; na
  - (vii) shughuli nyingine zinazohusiana na uratibu na kujiandaa kwa ajili ya kukabiliana na maafa yanayoweza kutokea.
- (c) katika kukabaliana na maafa yanapotokea, yafuatayo yatazingatiwa:
- (i) utoaji wa tahadhari ya mapema;
  - (ii) kufanya tathmini ya haraka ya madhara na mahitaji ya waathirika;
  - (iii) utafutaji na uokoaji na kuhamisha watu;
  - (iv) ugawaji wa misaada ya kibinadamu;
  - (v) ujenzi wa makazi ya muda;
  - (vi) kutoa elimu kwa umma kuhusu njia za kukabiliana na maafa yanayoweza kusababishwa na matokeo yake; na
  - (vii) shughuli nyingine zinazohusiana na uratibu na kukabiliana na maafa pale yanapotokea.
- (d) katika kurejesha hali baada ya maafa, yafuatayo yatazingatiwa:
- (i) kufanya tathmini ya mahitaji baada ya maafa;
  - (ii) kujenga upya miundombinu iliyoharibika sana;
  - (iii) kuhuisha kurejesha huduma za kiuchumi na kijamii ili kuboresha mifumo ya maisha ya eneo lililoathirika;
  - (iv) kutoa elimu kwa umma kuhusu njia za kurejesha hali kuwa bora zaidi; na
  - (v) shughuli nyingine zinazohusiana na uratibu na kurejesha hali baada ya maafa kutokea.
- (2) Matumizi ya fedha za Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa kwa shughuli zilizobainishwa

kwenye kanuni ndogo ya (1) (a) na (b) hayatazidi asilimia ishirini na tano kwa mwaka wa fedha husika.

Majukumu ya Serikali za Mitaa

12. Kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa itakuwa na jukumu la-

- (a) kuandaa programu za taarifa kwa umma kwa lengo la:
  - (i) kuelimisha umma kujilinda dhidi ya majanga;
  - (ii) kuelimisha umma kuhusu hatua za awali za kukabiliana na majanga katika makazi, maeneo ya umma au katika jamii;
  - (iii) kupunguza madhara, kuokoa maisha, kulinda mali na mazingira wakati wa matukio ya maafa; na
  - (iv) kuzuia matukio hatarishi kutofikia hatua ya kuwa maafa;
- (b) kutenga na kutambua maeneo maalum yatakayotumika kwa ajili ya makazi ya muda wakati wa maafa; na
- (c) kushughulikia na kuratibu dharura ambazo si maafa ya kitaifa.

Majukumu ya taasisi za Serikali

13. Isipokuwa kwa mujibu wa Sheria, kila taasisi ya serikali na taasisi ya kisekta inayojihusisha na shughuli za usimamizi wa maafa-

- (a) itachukua juhudi za makusudi na zinazofaa katika kuandaa mpango wa usimamizi wa maafa;
- (b) itaandaa na kutekeleza programu za mafunzo kwa watumishi wake na mtu mwingine kuhusiana na utoaji wa huduma muhimu na taratibu za kuzingatiwa wakati wa kukabiliana na maafa na kurejesha hali;
- (c) itatoa elimu kwa umma kuhusu vihatarishi kwa usalama na utayari wa kukabiliana na majanga;
- (d) wakati wa tukio la maafa:
  - (i) itagawa majukumu ya usimamizi wa maafa kwa wadau mbalimbali na

- kuratibu utekelezaji wake;
- (ii) itachukua hatua za haraka za kukabiliana na maafa na kutoa misaada;
- (iii) itawezesha upatikanaji na usambazaji wa bidhaa na huduma muhimu;
- (iv) itahakikisha uwepo wa mawasiliano ya kimkakati; na
- (v) itafanya jambo lolote linalotakiwa kwa kuzingatia programu za usimamizi wa maafa.

Mpango wa Usimamizi wa Maafa na Mpango wa Mwendelezo wa Huduma wakati wa Dharura ya Kitaifa

14.-(1) Mpango wa Usimamizi wa Maafa na Mpango wa Mwendelezo wa Huduma wakati wa Dharura ya Kitaifa uliyoandaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 10

(1) (f) cha Sheria utajumuisha yafuatayo-

- (a) taasisi mbalimbali na majukumu yao;
- (b) uwezo wa taasisi kukabiliana na dharura;
- (c) majukumu ya kiuratibu;
- (d) mpangilio wa kitaasisi;
- (e) matamko na udhibiti wa matukio ya maafa;
- (f) taratibu za kiutendaji;
- (g) taratibu za mawasiliano;
- (h) taratibu za tahadhari ya mapema;
- (i) huduma za kibinadamu kwa waathirika;
- (j) utafutaji wa rasilimali;
- (k) ufuatiliaji na tathmini;
- (l) huduma ya afya ya akili na kisaikolojia;
- (m) majaribio ya utayari wa kukabiliana na matukio ya maafa;
- (n) tathmini baada ya maafa;
- (o) uendelezaji wa tafiti, elimu na tathmini za usimamizi wa maafa;
- (p) ujuzi asilia unaohusu usimamizi wa maafa; na
- (q) mipango mingine ya kisekta iliyohuishwa kulingana na mahitaji.

(2) Pale ambapo Mpango wa Usimamizi wa Maafa wa Mwendelezo wa Huduma wakati wa Dharura hautakamilisha shughuli za kukabiliana na dharura iliyotokea, sekta husika zitawajibika kuzingatia hatua za kurejesha hali kuwa bora zaidi kwa kutenga bajeti katika

mwaka wa fedha unaofuata.

Ngazi za  
kushughulikia  
maafa

15.-(1) Kutakuwa na ngazi tatu za kushughulikia maafa kama ifuatavyo-

- (a) maafa ya ngazi ya wilaya endapo yataathiri wilaya moja pekee na kwamba, halmashauri iliyoathiriwa ina uwezo wa kukabiliana nayo bila kuhitaji msaada kutoka halmashauri nyingine au mamlaka nyingine za Serikali;
- (b) maafa ya ngazi ya mkoa endapo yataathiri zaidi ya Wilaya moja katika mkoa husika na kwamba, mkoa huo una uwezo wa kukabiliana nayo bila kuhitaji msaada kutoka mkoa mwingine au mamlaka nyingine za Serikali; na
- (c) maafa ya ngazi ya Taifa endapo yataathiri zaidi ya mkoa mmoja na kwamba, mikoa iliyoathiriwa haina uwezo wa kukabiliana nayo bila msaada kutoka ngazi ya taifa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), ngazi ya juu inaweza kushughulikia maafa yaliyojitokeza katika ngazi yoyote endapo kutakuwa na sababu mahsusi au kwa kuzingatia chanzo au ukubwa wa madhara yaliyojitokeza ili kukabili au kurejesha hali.

Tathmini ya  
eneo la maafa

16.-(1) Endapo kuna tishio au tukio la maafa Divisheni itaratibu yafuatayo-

- (a) kufanyika kwa tathmini ili kubaini ukubwa wa maafa;
- (b) uainishaji wa ngazi ya maafa kama ya kijiji/mtaa, kata, wilaya, mkoa au taifa; na
- (c) utunzaji wa kumbukumbu za madhara kwenye kanzidata ya matukio ya maafa.

(2) Wakati wa kuratibu tathmini ya ukubwa wa maafa, Divisheni itazingatia taarifa, mapendekezo na ushiriki wa kamati za kitaalam za usimamizi wa maafa za mikoa, wilaya, kata, kijiji au mtaa.

(3) Endapo maafa ni makubwa au madogo zaidi ya tathmini ya awali, Divisheni inaweza kuainisha upya ngazi ya maafa kama ya kijiji au mtaa, kata, wilaya, mkoa au

taifa baada ya kushauriana na kamati za usimamizi wa maafa katika ngazi husika.

Timu ya tathmini ya madhara na mahitaji

17.-(1) Mara tu baada ya maafa kutokea au kufuatia maombi ya Kamati ya Wataalam ya Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya mkoa, Divisheni itaratibu na kutuma timu ya tathmini kwenye eneo la maafa kwa lengo la kufanya tathmini ya mahitaji ya haraka na uharibifu.

(2) Timu ya tathmini itajumuisha wataalam ambao wataweza kukusanya taarifa muhimu zifuatazo-

- (a) taarifa za jumla kuhusu eneo la maafa;
- (b) kiwango na aina ya madhara;
- (c) mahitaji muhimu ya kimaisha kama vile chakula na lishe, malazi na huduma za afya;
- (d) mahitaji ya makundi maalum;
- (e) mahitaji ya maji na usafi wa mazingira;
- (f) mahitaji ya kielimu;
- (g) mahitaji ya majengo na miundombinu;
- (h) taratibu zinazoendelea katika kushughulikia maafa; na
- (i) taarifa zozote muhimu.

(3) Tathmini ya mahitaji ya haraka na uharibifu itafanyika kwa kuzingatia mwongozo wa tathmini ulioandaliwa na Divisheni.

Notisi ya kuondoka

18.-(1) Endapo itaonekana kuna haja ya wananchi kuondoshwa kutoka katika eneo la maafa, Waziri atatoa notisi kwa wananchi kuondoka katika eneo hilo na kuelekea katika eneo lililotengwa na kutambuliwa na Serikali kama makazi ya muda wakati wa maafa.

(2) Notisi ya kuondoka itakayotolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) itabainisha aina ya maafa, eneo linalotakiwa wananchi kuondoka na madhara yanayoweza kutokea kwa wananchi kama ilivyobainishwa kwenye Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

(3) Endapo notisi inatolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), Katibu Mkuu ataratibu shughuli za uondokaji wa wananchi kwa kushirikiana na Kamati za Usimamizi za Maafa na mamlaka na wadau wengine wanaohusika na dharura na usimamizi wa maafa

ikijumuisha Jeshi la Polisi Tanzania na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

(4) Kila mtu atapaswa kuzingatia notisi ya kuondoka iliyotolewa kwa mujibu wa kanuni hii, na endapo hatazingatia notisi hiyo atalazimishwa na mamlaka kuondoka katika eneo la maafa.

Notisi ya kurudi katika makazi ya awali au kwenda katika eneo salama

19.-(1) Endapo itaonekana inafaa, Waziri atatoa notisi ya kuwataka waathirika walio kwenye makazi ya muda kurudi katika makazi yao ya awali endapo yamethibitishwa kuwa ni salama baada ya maafa kutokea au kwenda eneo salama lililotengwa na Serikali kwa ajili ya makazi ya kudumu.

(2) Notisi itakayotolewa kwa mujibu wa kanuni (1) itabainisha eneo linalotakiwa wananchi kurudi kama ilivyobainishwa kwenye Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

(3) Kila mtu atapaswa kuzingatia notisi iliyotolewa kwa mujibu wa kanuni hii, na endapo hatazingatia notisi hiyo atalazimishwa na mamlaka kurudi katika makazi yake ya awali yaliyothibitishwa kuwa ni salama baada ya maafa kutokea, au kwenda katika eneo salama lililotengwa na Serikali kwama makazi ya kudumu.

Notisi ya kubaki katika sehemu ambapo mtu yupo

20.-(1) Endapo itaonekana kuwa kuna haja ya wananchi kubaki mahali walipo, Waziri atatoa notisi kwa wananchi hao kubaki mahali walipo kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

(2) Notisi ya wananchi kubaki mahali walipo itakayotolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) itabainisha aina ya janga na maafa yaliyotokea au yanayoweza kutokea, eneo linalotakiwa wananchi kubaki na madhara yanayoweza kutokea kwa wananchi endapo wataondoka katika eneo hilo.

(3) Endapo notisi inatolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), Katibu Mkuu ataratibu shughuli za wananchi kubaki mahali walipo kwa kushirikiana na kamati za usimamizi za maafa na mamlaka na wadau wengine zinazohusika na dharura na usimamizi wa maafa ikijumuisha Jeshi la Polisi Tanzania na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.



(4) Kila mtu atapaswa kuzingatia notiisi ya kubaki mahali alipo iliyotolewa kwa mujibu wa kanuni hii, na endapo hatazingatia notiisi hiyo atalazimishwa na mamlaka kubaki mahali alipo.

Notiisi ya kuendelea na shughuli za kijamii na kiuchumi

21.-(1) Endapo itaonekana inafaa, Waziri atatoa notiisi ya kumtaka mtu yeyote aliyetakiwa kubaki eneo alipo wakati wa maafa kuendelea na shughuli za kijamii na kiuchumi baada ya hali kuwa salama.

(2) Notiisi itakayotolewa kwa mujibu wa kanuni (1), itakuwa kama iliyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

#### SEHEMU YA NNE

#### UTARATIBU WA KUJITOLEA KATIKA USIMAMIZI WA MAAFA

Ushiriki wa wanaojitolea katika usimamizi wa maafa

22.-(1) Mtu yeyote, taasisi binafsi au shirika lisilo la kiserikali linaweza kujitolea kufanya yafuatayo-

- (a) kutoa au kusaidia utoaji wa huduma za usimamizi wa maafa katika mkoa, wilaya, kata, kijiji au mtaa; na
- (b) kufanya jukumu lolote linalohusiana na usimamizi wa maafa kama itakavyoelekezwa na kamati za usimamizi wa maafa za ngazi husika.

(2) Mtu yeyote, taasisi binafsi au shirika lisilo la kiserikali linalotaka kujitolea kutekeleza majukumu yaliyobainishwa katika kanuni ndogo ya (1), linawajibika kujaza fomu ya maombi iliyoainshwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi na kuiwasilisha kwa Katibu wa Kamati ya Usimamizi wa Maafa iliyopo katika ngazi husika kabla ya kujihusisha na shughuli ya usimamizi wa maafa.

(3) Endapo ombi la kujitolea lililowasilishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) litakubaliwa, mwombaji atapaswa kujaza fomu ya kiapo cha maadili cha kujitolea kwenye shughuli za usimamizi wa maafa kilichopo kwenye Jedwali la Nne la Kanuni hizi.

(4) Mtu, taasisi au shirika litakalojitolea, wakati wa matukio ya maafa litapaswa kuwa na vifaa muhimu kwa ajili ya kutekeleza shughuli hizo.

(5) Endapo mtu, taasisi au shirika linalojitolea wakati wa matukio ya maafa litakuwa halina vifaa muhimu, linaweza kupatiwa vifaa na mamlaka zinazohusika ili kutekeleza shughuli hizo, na vifaa hivyo vitaendelea kuwa mali ya mamlaka iliyovitoa.

(6) Mtu yeyote, taasisi binafsi au shirika lisilo la kiserikali litakalo kiuka kiapo cha maadili kilichobainishwa chini ya kanuni ndogo ya (3) litakuwa limetenda kosa na-

- (a) iwapo ni mtu ndiye ametenda kosa na akatiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kisichopungua mwezi mmoja na kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja.
- (b) iwapo ni taasisi binafsi au shirika lisilo la kiserikali ndiyo limetenda kosa na kutiwa hatiani, litalipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi laki tano au kufungiwa kujihusisha na shughuli za usimamizi wa maafa kwa muda usiopungua mwezi mmoja na usiozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Majibu ya ombi la kujitolea na ukomo wa kujitolea

23.-(1) Ombi la kujitolea kwenye shughuli za usimamizi wa maafa lililowasilishwa kwamujibu wa kanuni ya 22(2), litajibiwa kwa maandishi na Katibu wa Kamati ya Usimamizi wa Maafa katika ngazi husika ndani ya siku saba tangu tarehe ya kupokea ombi hilo, ikielezwa endapo mwombaji amekubaliwa au amekataliwa.

(2) Endapo mwombaji atakubaliwa kujitolea kwenye shughuli za usimamizi wa maafa, atahudumu katika shughuli hizo hadi pale ambapo-

- (a) ataacha kujitolea baada ya kutoa notisi ya siku saba kwa Katibu wa Kamati ya Usimamizi wa Maafa katika ngazi husika ikieleza nia yake ya kuacha kujitolea kwenye shughuli za usimamizi wa maafa;
- (b) atakiuka kiapo cha maadili ya kujitolea kwenye shughuli za usimamizi wa maafa alichokiapa

- kwa mujibu wa kanuni ya 22(3);
- (c) atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi unaotakiwa;
  - (d) atakaidi au atashindwa kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake kwenye Kamati ya Usimamizi wa Maafa baada ya kuelekezwa kufanya hivyo na kamati husika;
  - (e) atahama kutoka eneo alilokuwa anatekeleza majukumu yake na kuhamia eneo lingine ambako atawajibika kuomba upya kujitolea kwa Kamati ya Usimamizi wa Maafa ya eneo husika;
  - (f) atafariki; au
  - (g) itathibitishwa na daktari kuwa na matatizo ya kiafya yanayozuia kutekeleza majukumu yake.

Kuanzishwa na ushiriki wa klabu katika shughuli za usimamizi wa maafa

24.-(1) Mtu, kikundi au taasisi yoyote inaweza kuanzisha klabu au kikundi kwa lengo la kutoa elimu na kuhamasisha kuhusu usimamizi wa maafa na kujitolea kusaidia waathirika wakati wa maafa.

(2) Klabu au kikundi kitakachoanzishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), kitatakiwa kujitambulisha na kueleza shughuli zake kwenye Kamati ya Usimamizi wa Maafa katika ngazi husika.

#### SEHEMU YA TANO MASHARTI YA JUMLA

Utoaji wa taarifa

25.-(1) Kamati za usimamizi wa maafa zitakuwa na mamlaka ya kutoa taarifa zozote zinazohusiana na usimamizi wa maafa katika maeneo yao kwa kuzingatia Sheria.

(2) Mtu yeyote atakayetoa taarifa zinazohusiana na maafa bila ridhaa ya Kamati ya Usimamizi wa Maafa katika eneo husika, atakuwa ametenda kosa, na atawajibika iwapo atatiwa hatiani kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kisichopungua mwezi mmoja na kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2), taarifa itakayotolewa na mtu yeyote kwa nia njema ya

kutoa tahadhari ya janga haitasebakika kuwa ni kosa.

Masharti  
kuhusu  
ukusanyaji wa  
misaada na  
michango  
wakati wa  
maafa

26.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kushawishi, kukusanya au kutekeleza shughuli yoyote yenye lengo la kushawishi au kukusanya michango au misaada wakati wa maafa bila ridhaa ya Kamati ya Usimamizi wa Maafa ya eneo husika.

(2) Fedha au misaada yoyote iliyokusanywa au kutolewa kwa ajili ya shughuli za maafa, zitawasilishwa kwenye Kamati ya Usimamizi wa Maafa ya eneo husika kwa kuzingatia utaratibu ufuatao-

- (a) misaada ya vifaa au vyakula itahakikiwa na kuthibitishwa usalama wake na Kamati za maafa kwa kushirikisha mamlaka za usalama na udhibiti ubora katika ngazi husika;
- (b) misaada yoyote inayohusisha masuala ya afya, ithibitishwe usalama wake na mamlaka za afya katika ngazi husika kabla ya kupokelewa;
- (c) misaada ya fedha itaingizwa moja kwa moja kwenye akaunti ya Benki ya Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa kwa kila mchangiaji kuandika neno “maafa” likifuatiwa na jina la Wilaya maafa yalipotokea au aina ya janga;
- (d) endapo itahitajika, Katibu Mkuu atatoa kibali kwa mkoa na halmashauri husika kutumia akaunti ya matumizi mengineyo na kila mchangiaji atatakiwa kuandika neno “maafa” likifuatiwa na jina la wilaya husika iliyoathirika na janga na michango hiyo itatolewa taarifa kwenye Kamati ya Usimamizi wa Maafa katika ngazi husika na kupata kibali cha matumizi kutoka kwa Katibu Mkuu; na
- (e) ikiwa ni misaada ya fedha kwa njia ya uhawilishaji, fedha hiyo itapelekwa kwa wananchi kupitia akaunti ya Serikali ya Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa au akaunti ya matumizi mengineyo kwa mkoa na halmashauri iliyoithinishwa na Katibu Mkuu kutumika katika ngazi husika.

(3) Fedha au misaada iliyokusanywa kwa mujibu

wa kanuni ya 25 (2), kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa maafa itatumika kwa shughuli iliyokusudiwa na endapo-

- (a) fedha hizo zitatumika kwa shughuli za maafa na kubaki, zitawekwa kwenye Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa;
- (b) misaada mingine iliyokusanywa itatumika na kubaki, itapelekwa kwenye ghala la kuhifadhia misaada ya kibinadamu lililoanzishwa kwa mujibu wa kanuni ya 27 lililopo karibu na eneo la maafa au kama itakavyoelekezwa na Katibu Mkuu.

(4) Misaada ya fedha zitakazovuka miaka miwili ya fedha bila kutumika zitahamishiwa kwenye Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa.

(5) Wizara kupitia mwongozo inaweza kuweka utaratibu bora wa makusanyo, malipo ya fedha za misaada ya maafa na matumizi ya vifaa vya misaada ya kibinadamu kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

Ghala la kuhifadhia misaada ya kibinadamu

27.-(1) Kutakuwa na ghala la kuhifadhia misaada ya kibinadamu litakaloanzishwa na Wizara katika kila kanda au kwa kadri ya mahitaji.

(2) Ghala lililoanzishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), litasimamiwa na wizara kwa kushirikiana na mamlaka ya mkoa husika.

Rejesta ya kutoa na kupokea misaada ya kibinadamu

28.-(1) Itaandaliwa rejesta maalum kwa ajili ya kupokea na kutoa misaada ya kibinadamu.

(2) Misaada yote ya kibinadamu itakayopokelewa na kutolewa itaingizwa kwenye rejesta maalum ya Kamati ya Usimamizi wa Maafa katika ngazi husika.

(3) Wizara kupitia mwongozo inaweza kuweka utaratibu bora wa kupokea misaada ya maafa kila mara kwa kadiri itakavyoonekana inafaa.

Makosa na adhabu

29. Mtu yoyote atayekiuka masharti ya Kanuni hizi ambapo adhabu mahsusi haijatolewa, atakuwa anatenda kosa, na iwapo atatiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kisichopungua mwezi mmoja na kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Kufutwa kwa TS Na.

30. Kanuni za Usimamizi wa Maafa zinafutwa.

12 la mwaka  
2017

JEDWALI LA KWANZA  
(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 9(2))

TAARIFA YA TATHMINI YA MADHARA YA MAAFA NA MAHITAJI

1. Aina ya maafa.
2. Eneo lililoathirika (kwa ukubwa gani) ikijumuisha majina ya vijiji, kata, wilaya na mikoa.
3. Tarehe na muda wa tukio.
4. Idadi ya vifo (kwa kuzingatia jinsia, umri katika makundi na watu wenye ulemavu).
5. Idadi ya majeruhi (kwa kuzingatia jinsia, umri katika makundi na watu wenye ulemavu).
6. Idadi ya watu waliookolewa, waliopotea na waliohamishwa.
7. Idadi ya kaya zilizoathirika na idadi ya waathirika (kwa kuzingatia jinsia, umri katika makundi na watu wenye ulemavu).
8. Idadi ya makazi yaliyoathirika (nyumba zilizobomoka kabisa na zilizoathirika kiasi).
9. Idadi ya waliopoteza makazi (kwa kuzingatia jinsia, umri katika makundi na watu wenye ulemavu).
10. Idadi ya watu walioathirika kwa namna nyingine na aina ya madhara (kwa kuzingatia jinsia, umri katika makundi na watu wenye ulemavu).
11. Idadi ya mifugo waliokufa au walioathirika.
12. Uharibifu wa mazao (aina ya mazao na ukubwa wa eneo kwa ekari/hekta).
13. Uharibifu wa miundombinu na kiwango cha uharibifu (barabara, madaraja, reli, nishati, mawasiliano, viwanda, usambazaji wa maji, majengo ya serikali, shule, vituo vya afya, kilimo n.k) na kiwango cha hasara na gharama za kurejesha hali.
14. Aina ya misaada inayohitajika kama vile:
  - (a) Huduma za afya na saikolojia;
  - (b) Misaada ya kibinadamu kama vile:
    - (i) Mablanketi;
    - (ii) makazi
    - (iii) chakula;
    - (iv) maji;
    - (v) mavazi.
  - (c) dawa na vifaa tiba ikiwemo chanjo, madawa ya kutibu maji, madawa ya binadamu na mifugo
  - (d) vifaa vya huduma kama vile:
    - (i) viti vya wagonjwa,
    - (ii) malori/ mabasi;
    - (iii) ndege;
    - (iv) Boti au mitumbwi.
  - (e) programu za ukarabati na kujenga upya.
15. Hali ya hewa ya eneo la maafa.
16. Vifaa vinavyohitajika kama vile redio, jenereta, visafishaji maji na matanki ya maji.
17. Fedha zinazohitajika kulipia gharama mbalimbali ikiwemo usafiri wa ndani, upakuaji wa vifaa na kuhifadhi sehemu salama.
18. Aina na kiasi cha vifaa vinavyoweza kununuliwa ndani ya nchi.
19. Aina na kiasi cha vifaa vya huduma za kibinadamu vinavyohitajika kutoka nje ya nchi pamoja na maelekezo ya namna ya usafirishaji kama vile njia inayopaswa

*Kanuni Za Usimamizi Wa Maafa*

*Tangazo la Serikali Na. 658A (Linaendelea.)*

- kutumika (anga au maji), nyaraka zinazohitajika kwa kibali cha haraka cha forodha na vyeti vya afya vinavyohitajika.
20. Kipindi cha dharura kinachotarajiwa (kwa kawaida isizidi miezi 3).
21. Hatua zilizochukuliwa na Kamati ya Usimamizi wa Maafa katika ngazi husika.
- (a) .....
- (b) .....
- (c) .....
22. Taasisi, mashirika na wadau wanaotoa huduma za kibinadamu za hiyari
- (a) .....
- (b) .....
- (c) .....
23. Aina ya mchango uliopokelewa na jina la mchangiaji au mfadhili
- (a) .....
- (b) .....
- (c) .....
24. Changamoto au mapungufu yaliyojitokeza wakati wa kukabili maafa.
25. Maoni na mapendekezo ya jumla.
26. Chanzo cha maelezo ya tukio.

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(1) (a); 18(2); 19(2); 20(1) na 21(2))*

*SEHEMU A*

**TANGAZO LA KUONDOKA KATIKA ENEO LA MAAFA AU HATARISHI**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(1) (a) na (ii))*

Kutokana na kutokea kwa janga la (taja aina ya janga lililotokea) .....  
tarehe.....mwezi.....20.....Saa.....katika eneo la.....(taja  
eneo husika lililoathiriwa na maafa), na kwa kuzingatia Notisi ya Kuondoka iliyotolewa  
tarehe.....mwezi.....20....., watu wote mliopo katika eneo hilo mnatangaziwa kuwa, hadi  
tarehe.....mwezi.....20.....Saa....alfajiri/asubuhi/mchana/alasiri/jioni/usiku,  
mnatakiwa kuwa mmeondoka katika eneo hilo na kuelekea eneo lililotengwa kwa ajili ya makazi ya  
muda litwalo.....

Endapo mtu yeyote atakiuka tangazo hili, ataondolewa kwa nguvu na mamlaka za serikali ili  
kunasuru maisha yake na ya wengine.

Imetolewa na (Jina la Waziri):.....

Cheo chake:.....

Sahihi:.....

Tarehe:.....

*SEHEMU B*

NOTISI YA KUONDOKA KATIKA ENEO LA MAAFA/HATARISHI  
(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 18(1) na (2))

Kutokana na kutokea kwa janga la (taja aina ya janga lililotokea) .....  
tarehe.....mwezi.....20.....Saa.....katika eneo la.....(taja  
eneo husika lililoathiriwa na maafa), watu wote waliopo katika eneo hilo mnaelekezwa kuwa, hadi  
kufikia  
tarehe.....mwezi.....20.....Saa.....alfajiri/asubuhi/mchana/alasiri/jioni/usiku,  
mnatakiwa kuwa mmeondoka katika eneo hilo na kuelekea eneo lililotengwa kwa ajili ya makazi ya  
muda liitwalo.....

Endapo mtu yeyote atakiuka tangazo hili, ataondolewa kwa nguvu na mamlaka za serikali ili  
kunasuru maisha yake na ya wengine.

Imetolewa na (Jina la Waziri):.....

Cheo chake:.....

Sahihi:.....

Tarehe:.....



*Kanuni Za Usimamizi Wa Maafa*

*Tangazo la Serikali Na. 658A (Linaendelea.)*

*SEHEMU C*

**NOTISI YA KURUDI KATIKA MAKAZI AU ENEO SALAMA**

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 19(1) na (2))*

Kutokana na kutokea kwa janga la (taja aina ya janga lililotokea) .....  
tarehe.....mwezi.....20.....Saa.....katika eneo la.....(taja  
eneo husika lililoathiriwa na maafa), watu wote waliopo katika eneo la makazi ya muda  
mnaelekezwa kuwa, hadi kufikia  
tarehe.....mwezi.....20.....Saa.....alfajiri/asubuhi/mchana/alasiri/jioni/usiku,  
mnatakiwa kuwa mmerudi katika makazi yenu ya awali kwa kuwa yamethibitishwa kuwa ni salama  
au kuelekea eneo lililotengwa kwa ajili ya makazi ya kudumu  
lililopo.....

Endapo mtu yeyote atakiuka tangazo hili, ataondolewa kwa nguvu na mamlaka za serikali kurudi  
katika makazi yake ya awali au kwenda eneo salama lililotengwa na serikali kwa ajili ya makazi ya  
kudumu.

Imetolewa na (Jina la Waziri):.....

Cheo chake:.....

Sahihi:.....

Tarehe:.....

*Kanuni Za Usimamizi Wa Maafa*

*Tangazo la Serikali Na. 658A (Linaendelea.)*

*SEHEMU D*

TANGAZO LA KUSIMAMISHA AU KUZUIA UUZAJI WA VILEO, VINYWAJI, SILAHA AU VITU VINGINE KATIKA ENEO LA MAAFA AU ENEO HATARISHI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(1)(a)(ii))*

Kutokana na kutokea kwa janga la (taja aina ya janga lililotokea) .....  
tarehe.....mwezi.....20.....Saa.....katika eneo la.....(taja  
eneo husika lililoathiriwa na maafa), watu wote waliopo katika eneo hilo mnatangaziwa kuwa, ni  
marufuku kuuza.....(taja kitu kinachozuliwa) kuanzia  
tarehe.....mwezi.....20.....Saa.....alfajiri/asubuhi/mchana/alasiri/jioni/usiku, hadi  
itakavyotangazwa vinginevyo.

Endapo mtu yeyote atakiuka tangazo hili, atalazimishwa na mamlaka za serikali kutii marufuku  
hiyo ili kunusuru maisha yake nay a wengine.

Imetolewa na (Jina la Waziri):.....

Cheo chake:.....

Sahihi:.....

Tarehe:.....

*SEHEMU E*

NOTISI YA KUTOONDOKA AU KUBAKI SEHEMU MTU ALIPO  
*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 20(1) na (2))*

Kutokana na kutokea kwa janga la (taja aina ya janga lililotokea) .....  
tarehe.....mwezi.....20.....Saa.....katika eneo la.....(taja  
eneo husika lililoathiriwa au linalotarajiwa kuathiriwa na maafa), mtu yeyote aliyepo katika eneo  
la.....(taja eneo ambalo mtu hapaswi kuondoka) hauruhusiwi kuondoka  
katika eneo alipo hadi itakavyoelekezwa vinginevyo.

Endapo mtu yeyote atakiuka notisi hii, atalazimishwa na mamlaka za serikali kubaki katika eneo  
alipo ili kunusuru maisha yake na ya wengine.

Imetolewa na (Jina la Waziri):.....

Cheo chake:.....

Sahihi:.....

Tarehe:.....

*Kanuni Za Usimamizi Wa Maafa*

*Tangazo la Serikali Na. 658A (Linaendelea.)*

*SEHEMU F*

NOTISI YA KUENDELEA NA SHUGHULI ZA KIJAMII NA KIUCHUMI BAADA YA NOTISI  
YA KUBAKI SEHEMU MTU ALIPO  
(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 21(1) na (2))

Kutokana na kutokea kwa janga la (taja aina ya janga lililotokea au lililotarajiwa kutokea)  
..... tarehe.....mwezi.....20.....Saa.....katika eneo  
la.....(taja eneo husika lililoathiriwa au lililotarajiwa kuathiriwa na maafa), mtu yeyote  
aliyekuwepo katika eneo la.....(taja eneo ambalo mtu hakupaswa  
kuondoka) ambaye alitakiwa kubaki eneo alipo wakati wa maafa, anatakiwa kuendelea na shughuli  
za kijamii na kiuchumi baada ya hali kuwa salama.

Imetolewa na (Jina la Waziri):.....

Cheo chake:.....

Sahihi:.....

Tarehe:.....

*Kanuni Za Usimamizi Wa Maafa*

*Tangazo la Serikali Na. 658A (Linaendelea.)*

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 22(2))*

FOMU YA MAOMBI YA KUJITOLEA  
KWENYE SHUGHULI ZA USIMAMIZI WA MAAFA

**1. Mtu**

- (a) Jina kamili.....
- (b) Jinsi.....
- (c) Umri.....
- (d) Uraia.....
- (e) Namba ya kitambulisho (NIDA, pasi ya kusafiria, leseni ya udereva, kitambulisho cha mpiga kura au utambulisho wowote).....
- (f) Anuani ya posta.....
- (g) Namba ya simu.....
- (h) Jina la mwajiri (kama yupo).....
- (i) Aina ya ajira (kama ipo).....
- (j) Aina ya huduma/kazi/utaalam/vifaa/shughuli ambayo mwombaji anatarajiwa kujitolea katika usimamizi wa maafa.....

.....  
Saini ya mwombaji

.....  
Tarehe

**2. Taasisi binafsi/Shirika lisilo la kiserikali**

- (a) Jina la Taasisi binafsi/Shirika lisilo la kiserikali.....
- (b) Namba ya usajili.....
- (c) Aina ya huduma zinazotolewa kwa kuzingatia hali ya usajili.....
- (d) Aina ya huduma/kazi/shughuli ambayo mwombaji anatarajiwa kujitolea katika usimamizi wa maafa.....

.....  
Saini ya mwombaji

.....  
Cheo

.....  
Tarehe

**3. Kwa matumizi ya Kamati ya Usimamizi wa Maafa katika ngazi husika**

- (a) Tarehe ombi lilipopokelewa.....
- (b) Jina na namba ya simu ya mtu aliyepokea.....
- (c) Jibu/uamuzi kuhusu ombi lilipopokelewa (mwombaji amekubaliwa/amekataliwa).....

.....  
Saini ya mtoa uamuzi

.....  
Cheo

.....  
Tarehe

*Kanuni Za Usimamizi Wa Maafa*

*Tangazo la Serikali Na. 658A (Linaendelea.)*

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 22(3))*

KIAPO CHA MAADILI KATIKA KUJITOLEA  
KWENYE SHUGHULI ZA USIMAMIZI WA MAAFA

Mimi.....(jina la mwombaji aliyekubaliwa ombi lake), kwa hiyari yangu bila kushurutishwa na mtu yeyote naapa/nathibitisha kwamba niko tayari kujitolea katika shughuli za usimamizi wa maafa katika eneo la.....(taja eneo husika) kwa kuzingatia yafuatayo: -

1. Sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya usimamizi wa maafa na sheria nyingine za Nchi.
2. Nitatoa huduma za kujitolea kwa weledi bila woga, upendeleo au huba kwa nitakaokuwa nawahudumia.
3. Nitatekeleza majukumu yangu chini ya uangalizi na usimamizi wa Kamati ya Usimamizi wa Maafa iliyopo katika eneo langu.
4. Sitatekeleza majukumu yangu kama wakala wa aina yoyote ile na badala yake nitatekeleza majukumu yangu kwa nafasi ya kujitolea kama nilivyoomba na kukubaliwa.
5. Sitatoa taarifa zozote au maoni kupitia vyombo vya habari kuhusu shughuli nitakazokuwa natekeleza isipokuwa kwa idhini ya Kamati ya Usimamizi wa Maafa ya eneo langu.
6. Nitatekeleza majukumu yangu kwa uaminifu bila kumbagua mtu yeyote kwa misingi ya rangi, hali ya mtu, dini, umri, jinsi, historia au asili ya mtu.
7. Na kwamba, kwa kiapo hiki nathibitisha kuwa hakuna udanganyifu, makosa ya kimantiki au ushawishi wowote kwangu na niko tayari kuwajibika mimi mwenyewe endapo itathibitika kuwa nilidanganya au nilishawishiwa vinginevyo kuhusiana na maelezo niliyoyatoa katika kiapo hiki.

NA NINATAMKA NA KUAPA/KUKIRI kiapo hiki nikiwa na akili timamu nikiamini kwamba, yote niliyoyaapa/niliyokiri katika kiapo hiki ni kweli, kweli tupu.

KIAPO HIKI KIMEAPWA ..... na  
..... ambaye namfahamu  
mimi mwenyewe /ametambulishwa kwangu na  
.....  
ambaye namfahamu mimi mwenyewe  
leo tarehe .....mwezi wa.....20....

.....  
MUAPAJI

MBELE YANGU:

JINA: .....

SAHIHI:.....

ANUANI: .....

WADHIFA: Mwenyekiti wa Kamati ya Usimamizi wa Maafa

Dodoma,  
21<sup>st</sup> Novemba, 2022

GEORGE BONIFACE SIMBACHAWENE  
Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu-  
Sera, Bunge na Uratibu